**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Dhima za Tasifida Kimuktadha katika Nyimbo za Singeli: Mifano kutoka kwa Msanii Msaga Sumu na Manfongo

*Baraka Sikuomba[1*] na Lina Godfrey[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, S. L. P. 35091. Dar es Salaam Tanzania
[*] ORCID ID: https://orcid/0009-0002-0563-3272; Barua pepe ya mawasiliano: 1987baraka@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1470**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*27 Septemba 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Tasifida, Singeli na Muktadha.*

**IKISIRI**

Kutokana na ufinyu wa tafiti zilizofanyika kuhusu tasifida katika muktadha wa nyimbo za singeli kumejengeka mtazamo hasi hasa kwenye lugha inayotumika katika muktadha wa nyimbo za singeli miongoni mwa wanajamii. Kutokana na umuhimu wa tasifida katika kuendeleza utamaduni wa jamii kulikuwa na haja ya kuchunguza na kuweka bayana dhima za matumizi ya tasifida katika nyimbo za singeli. Kwa hiyo, makala hii imeangalia dhima za tasifida kimuktadha katika nyimbo za singeli kwa kutumia nyimbo ziitwazo "Siponaye", "Dada Asha", "Spesho", "Mtoto Mdogo" za msanii Msaga Sumu na "Chawa", "Hainogi", "Kitasa", "Mashine" "Kipusa", "Muacheni Adange" za msanii Manfongo. Nadharia ya Semiotiki imetumika kufafanua dhima za tasifida katika nyimbo za wasanii teule. Katika nyimbo hizo tasifida mbalimbali zimetumiwa na wasanii teule kuwasilisha maudhui yao. Nyimbo hizi za singeli, licha ya kuimbwa kwa lugha inayoonekana ni ya mtaani, zimezingatia sana matumizi ya tasifida katika kupunguza ukali wa maneno. Matokeo ya utafiti huu yameonesha wazi kuwa matumizi ya lugha ya tasifida katika nyimbo za singeli, yameonesha wazi kwamba nyimbo za singeli zina dhima kadha wa kadha zinazowasilishwa kwa njia ya matumizi ya tasifida. Kupitia matumizi ya tasifida katika nyimbo za singeli, ni bayana kwamba tasifida zina dhima za msingi katika nyimbo za singeli katika kuendeleza mila, utamaduni na desturi za mawasiliano katika jamii. Dhima hizo ni pamoja na kubainisha kazi zisizo halali katika jamii, kuibua tabia zisizokubarika katika jamii, kukemea mmomonyoko wa maadili katika jamii, kuhimiza umuhimu wa mapenzi ya dhati katika jamii na kuweka bayana uhalisia wa mwanaume. Hivyo basi, watafiti wengine wanaweza kufanya utafiti kama huu kwa kuchunguza kwa kina tofauti ya tasifida na taswira kimuktadha katika nyimbo teule za utafiti huu.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1470

**APA CITATION**

Sikuomba, B. & Godfrey, L. (2023). Dhima za Tasifida Kimuktadha katika Nyimbo za Singeli: Mifano kutoka kwa Msanii Msaga Sumu na Manfongo. *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 382-393. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1470.

**CHICAGO CITATION**

Sikuomba, Baraka and Lina Godfrey. 2023. "Dhima za Tasifida Kimuktadha katika Nyimbo za Singeli: Mifano kutoka kwa Msanii Msaga Sumu na Manfongo". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 382-393. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1470.

**HARVARD CITATION**

Sikuomba, B. & Godfrey, L. (2023) "Dhima za Tasifida Kimuktadha katika Nyimbo za Singeli: Mifano kutoka kwa Msanii Msaga Sumu na Manfongo", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 382-393. doi: 10.37284/jammk.6.1.1470.

**IEEE CITATION**

B. Sikuomba & L. Godfrey "Dhima za Tasifida Kimuktadha katika Nyimbo za Singeli: Mifano kutoka kwa Msanii Msaga Sumu na Manfongo", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 382-393, Sep. 2023.

**MLA CITATION**

Sikuomba, Baraka & Lina Godfrey. "Dhima za Tasifida Kimuktadha katika Nyimbo za Singeli: Mifano kutoka kwa Msanii Msaga Sumu na Manfongo". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Sep. 2023, pp. 382-393, doi:10.37284/jammk.6.1.1470.

## UTANGULIZI

Wataalamu mbalimbali wamefanya tafiti zao kuhusu tasifida katika kazi mbalimbali za kifasihi. Mathalani, Khatibu (1986) anaeleza kuwa tasifida inapotumika katika fasihi hujenga itifaki nzuri. Si hivyo tu, wapo waliochunguza matumizi ya tamathali za semi katika nyimbo na kubaini kuwa tasifida husaidia kupunguza ukali au utusi. Badala ya kutumia neno, msemo au nahau kali ama ya utusi, tasifida hutumika (Yangi, 2015). Pamoja na tasifida kuwa na umuhimu katika kazi mbalimbali za kifasihi kama ilivyobainishwa, uchunguzi wa kutosha kuhusu dhima za tasifida kimuktadha katika nyimbo za singeli za wasanii teule haujafanywa. Kutochunguzwa kwa dhima za tasifida kumeacha ombwe lililowaibua wanazuoni wanaodai kuwa nyimbo za singeli hazina maadili. Mathalani, Mwanisenga (2017) anaeleza kuwa nyimbo za singeli ni nyimbo ambazo hazina maadili kwa sababu ukisikiliza mashairi yake ni lazima ugeuke nyuma uangalie unasikiliza na nani. Naye Zahoro (2018) anaeleza kuwa nyimbo za singeli huonekana zinatumia lugha ya kihuni. Mahitimisho kuhusu nyimbo za singeli yaliyotolewa na wanazuoni Mwanisenga na Zahoro ni ya jumla sana. Kutokana na umuhimu wa tasifida katika singeli makala hii imechunguza dhima za tasifida katika nyimbo za singeli kulingana na muktadha wa ujitokezaji wake. Lengo la makala hii ni kuonesha kuwa singeli hazitumii lugha ya kiuni bali lugha inayotumika inalenga kudumisha uhusiano na kuonesha uhalisia uliomo katika jamii na maisha ya binadamu kwa ujumla.

## NADHARIA YA UTAFITI

Nadharia ni mwongozo, utaratibu, kanuni, sheria na miiko ambayo humwongoza mtu katika kulifahamu jambo vile lilivyo au linavyotakiwa liwe (Babbie, 1999). Katika utafiti huu, mtafiti alitumia nadharia ya Semiotiki ili kuweza kufikia malengo ya utafiti pamoja na kujibu maswali ya utafiti huu. Semiotiki ni nadharia inayohusika na uchambuzi wa masuala ya lugha inayotokana na nadharia ya Umuundo iliyoasisiwa na Ferdinand de Saussure (1966). Kuzuka kwa nadharia ya Semiotiki kunahusishwa na miaka ya 1970 wakati ambapo kulikuwa na mwelekeo mkubwa wa kuuasi na kuuacha umuundo uliokuwa umeutawala uhakiki wa kifasihi katika miaka ya 1960. Uasi wa kuachana na umuundo ulitokana na wanamiundo kujikita zaidi katika kuhakiki na kufafanua miundo ya lugha katika mawasiliano ya kijamii badala ya kubainisha wazi uhusiano uliopo baina ya matumizi ya miundo hiyo kama ishara na kile ambacho huwakilishwa katika utamaduni wa jamii (Ndungo, 2006).

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1470

Ferdinand de Saussure (1966) anaeleza kwamba neno "Semiotiki" limenyambuliwa kutokana na neno la Kigiriki *semeion* lenye maana ya ishara linalowakilisha vikundi vya wafuasi wa mielekeo fulani. Mwasisi wa nadharia hii ni Ferdinand de Saussure ambaye katika kitabu chake cha *Course in General Linguistic* alipendekeza neno la kisayansi lililoitwa *semiology*. Kuanzia hapo Semiotiki na Semioloji yakawa ndiyo maneno mbadala yanayotumika kujifunza ishara katika shughuli za binadamu. de Saussure (1966) ameeleza kuwa katika lugha huwa kuna vitu viwili, yaani 'kitaja' ambalo ni jina linalotaja kitu fulani na 'kitajwa' ambacho ni kile kinachorejelewa na jina hilo. Hata hivyo, de Saussure (1966) anasisitiza kuwa katika hali ya kawaida hakuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya kitaja na kitajwa bali uhusiano uliopo ni wa kidhahania tu. Maelezo ya de Saussure yanaungwa mkono na Blonsky (1991) anayeeleza kuwa mahusiano yaliyopo baina ya kitaja na kitajwa ni mahusiano dhahania isipokuwa kwa baadhi ya vitu ambavyo majina yake hutokana na mlio wake. Peirce (1997) amezungumzia maana halisi ya lugha ya ishara inavyohusiana kimantiki na utamaduni wa jamii fulani kwa madhumuni ya kutoa maana maalumu. Hivyo, nadharia ya Semiotiki ndiyo inayohusika katika kuchunguza matumizi ya lugha ya ishara na uashiriaji katika kazi za fasihi (Chandler, 2002). Si hivyo tu, bali pia nadharia hii hushughulikia lugha ya picha na ishara kwa sababu watumiaji wa lugha huweza kutumia neno fulani lakini maana waliyoimaanisha ikawa si ile inayohusika na neno hilo (Silavwe, 2016).

Kwa hiyo, ili nadharia ya Semiotiki ikamilike, ni lazima mawazo ya Roland Barthes (1994) kuhusu misimbo mitano ya usomaji iliyoleta athari kubwa katika uhakiki wa ishara na uashiriaji kwenye kazi za kifasihi yarejelewe. Misimbo iliyotolewa na Barthes ndiyo nguzo kuu za nadharia ya Semiotiki. Barthes anaeleza kuwa matumizi ya lugha ya kiishara na uashiriaji katika kazi za fasihi hujitokeza katika misimbo ya aina tano ambayo imefafanuliwa hapa chini:

Msimbo wa kwanza ni wa kimatukio. Huu ni msimbo ambao unahusu jinsi matukio yanayopatikana katika hadithi au masimulizi yanavyofuatana na namna msomaji anavyoweza kuelewa msuko wa kazi husika ya kifasihi kwa kuzingatia jinsi matukio yanavyoambatana kiusababishi. Msanii wa kazi ya fasihi anaweza kujenga visa na matukio katika kazi yake ya kifasihi kwa kutumia njia ya msimbo wa kimatukio.

Msimbo wa pili ni wa ki-seme. Neno 'seme' hutumiwa kueleza elementi nasibihi ya kisemantiki. Semantiki ni taaluma inayoshughulikia maana za maneno katika lugha ya mwanadamu ambapo maneno huwa na maana ya msingi na maana ya ziada (Barthes, 1994). Maana ya msingi ni ile ambayo inaweza kutumika na kurejelewa katika muktadha rasmi, wakati maana za ziada za maneno hutumika katika muktadha usio rasmi. Msimbo wa kiseme hutumiwa na wahakiki na wanafasihi katika kujenga dhamira au maudhui kwa kutumia maneno yanayotoa ukaribu wa maana ya msingi ya neno na kile kinachorejelewa na neno hilo katika kazi husika ya kifasihi.

Msimbo wa tatu ni wa kiishara. Msimbo wa kiishara wa nadharia ya Semiotiki huwasaidia watafiti na wahakiki wa kazi ya kifasihi kubainisha lugha ya ishara inayotumika katika kazi ya fasihi kiasi cha kuweza kutambua dhamira katika kazi yoyote ya kifasihi.

Msimbo wa nne ni wa kiurejelezi ambao hujengwa kutokana na viashiria vya kiutamaduni ambavyo vinarejelewa katika kazi za kifasihi. Msimbo huu mara nyingi huhusisha matumizi ya vitu au dhana zinazoeleweka kwa wasomaji na hivyo kuifanya kazi fulani ya kifasihi kuwa na nguzo ya kiutamaduni ambapo mtunzi hutumia hulka au mila na desturi na wakati mwingine imani katika kuiwasilisha kazi yake.

Msimbo wa tano ni wa kihemetiki ambao ni msimbo unaohusu taharuki na hujulikana kama msimbo wa kusimulia au kutamba hadithi. Hata hivyo si

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1470

misimbo yote iliyorejelewa katika makala haya isipokuwa msimbo wa kiurejelezi kwani ndio uliokidhi na kufanikisha lengo la Makala haya.

## Historia Fupi ya Wasanii Teule

Sehemu hii inahusu historia fupi ya wasanii Selemani Jabiri pamoja na Amani Hamisi katika nyimbo za singeli.

### *Selemani Jabiri (Msaga Sumu)*

Selemani Jabiri alizaliwa katika kijiji cha Mtama, mkoa wa Lindi mwaka 1981. Katika familia yao, yeye ni mtoto wa kwanza kati ya watoto sita. Kielimu, hakuweza kuhitimu masomo ya sekondari kutokana na kipato cha wazazi wake kuwa chini. Hali hii, ilisababisha ashindwe kujikimu mahitaji yake ya shule. Aidha, yeye ni miongoni wa waanzilishi wa kwanza wa nyimbo za singeli katika miaka ya 2010 ambapo alikuwa akiimba na wenzake kwenye sherehe za kukesha mtaani. Mbali na kujishughulisha na muziki wa singeli, Selemani Jabiri (Msaga Sumu) anajishughulisha na biashara ya mitumba katika soko la Tandale, jijini Dar es Salaam. Msanii Selemani Jabiri (Msaga Sumu) mpaka sasa ana nyimbo 44 ambazo ni: ‘Nasaka Riziki’ (2016), ‘Kidole Changu’ (2016), ‘Matobo’ (2016), ‘Jirani’ (2016), ‘Tatizo Nyota’ (2016), ‘Mambo Bado’ (2016), ‘Mwacheadange’ (2017), ‘Maisha’ (2017), ‘Lowasa’ (2017), ‘Usije Mjini’ (2018), ‘Kitu Gani’ (2018), ‘Niseme Nisiseme’ (2018), ‘Maua’ (2018), ‘Kitu Gani’ (2018), ‘Popo’ (2018), ‘Umepenya’ (2018) ‘Majonzi’ (2019), ‘Uwani’ (2019), ‘Kofia’ (2019), ‘Yanga’ (2019), ‘Dunia Imebadilika’ (2019), ‘Achimenengule’ (2019), ‘Simba’ (2019), ‘Mbwi’ (2019), ‘Babu wa Ruanga’ (2020), ‘Mchawi Pes’ (2020), ‘Tucheze’ (2020), ‘Kama ipo ipo’ (2020), ‘Mama wa Kambo’ (2020), Kizibo;’ (2020), ‘Magufuli’ (2020), ‘Dodoki’ (2020), ‘Kafuata Zigo Langu la Singeli’ (2021), ‘Mwanaume Mashine’ (2021), ‘Nimerudi’ (2021), ‘Talaka’ (2021), ‘Sielewi’ (2021), ‘Kitasa’ (2021), ‘Njaa Kali’ (2021), ‘Rafiki wa Kweli’ (2021), ‘Kipusa’ (2021), ‘Mama Ntilie’ (2021), ‘Naomba Kuingia’ (2021) na ‘Unanitega Shemeji’ (2021).[1]

### *Amani Hamisi (Manfongo)*

Amani Hamisi alizaliwa 1992 katika kata ya Tandale, wilaya ya Ubungo, jijini Dar es Salaam. Ni mtoto wa kwanza kati ya watoto watatu katika familia yao. Kielimu, Amani Hamisi ameishia darasa la saba. Alianza kujishughulisha na muziki wa Singeli mwaka 2016 ambapo alitambulishwa zaidi na wimbo wake unaojulikana kwa jina la “Hainaga Ushemeji Tunakulaga”. Mpaka sasa msanii Amani Hamisi (Manfongo) ameimba nyimbo 38 ambazo ni ‘Nani Bado Sijamtaja’ (2016), ‘Hauna’ (2016), ‘Nakula Ujana’ (2016), ‘Hainaga Ushemeji’ (2016), ‘Kibaka’ (2016), ‘Hauna kila Kitu’ (2016), ‘Sio Poa’ (2016), ‘Kimya Kimya’ (2017), ‘Zali la Mwanaspoti’ (2017), ‘Ndondo Cup’ (2017), ‘;Kisingeli Singeli’ (2017), ‘Ataweza’ (2017), ‘Lau Nafasi’ (2017), ‘Safi Tu’ (2017), ‘Asiependa Kujinafasi’ (2017), ‘Navimba’ (2018), ;’Twitter’ (2018), ‘Toto’ (2018), ‘Mwenye Donge Ameze’ (2018), ‘Mjeda’ (2018), ‘Bata Mzinga’ (2018), ‘Spesho’ (2018), ‘Pangusa’ (2019), ‘Longa’ (2019), ‘Chungu Tamu’ (2019), ‘Sipo Naye’ (2020), ;’Matepeli’ (2020), ‘Pisi Kali’ (2020), ‘Ndio Basi Tena’ (2021), ‘Rudi’ (2021), ‘Hainogi’ (2021), ‘Yeye’ (2021), ‘Chawa’ (2021), ‘Kibwana – Asha’ (2021), ‘Mtoto mdogomdogo’ (2021), ‘Bwaga’ (2021) na ‘Kama Vocha’ (2021).[2]

## METHODOLOJIA

Utafiti huu ulikuwa wa kimaktaba. Kwa kuwa utafiti huu ni wa kiuchambuzi, uliegemea zaidi katika mtandao wa YouTube. Kwa mantiki hiyo, data za makala hii zilikusanywa kutoka katika nyimbo za singeli za msanii Msaga Sumu na Manfongo zilizohifadhiwa katika mtandao wa YouTube. Jumla ya nyimbo 11 ziliteuliwa ili

[1]Taarifa hizi zimedondolewa kutoka katika kipindi cha Mkasi kinachopatikana youtubehttps://youtube.be//21QX9ljuc.

[2]Taarifa hizi zimedondolewa kutoka katika kipindi cha Global Tv kinachopatikana youtubehttps://youtube.be/fOUxszd4T1.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1470

kuweza kufikia malengo ya makala hii. Aidha, katika jumla ya nyimbo 11, nyimbo 6 zilikuwa za msanii Manfongo ambazo ni pamoja na Siponaye", "Dada Asha", "Spesho", "Chawa", "Hainogi", na "Mtoto Mdogo" wakati nyimbo 5 zilikuwa za msanii Msaga Sumu ambazo ni pamoja na "Kipusa" "Muacheni Adange", "Kitasa", na "Mashine". Uteuzi wa nyimbo hizo umezingatia kipindi ambacho jamii ilianza kupata ufahamu kuwa nyimbo za singeli hususan zilizoteuliwa katika utafiti huu si za wahuni, wezi, na wagomvi bali ni nyimbo ambazo Watanzania wanapaswa kujivunia kuliko aina nyingine za nyimbo ambazo zina Uzunguuzungu mwingi (Zahoro, 2018). Aidha, tulitumia mbinu ya usampulishaji nasibu sahili. Huu ni usampulishaji ambao watafitiwa huwa na nafasi sawa ya kuchaguliwa. Kwa hiyo, mtafiti aliandika kwenye vikaratasi nyimbo zote za wasanii teule walizoimba kati ya mwaka 2017 hadi 2021, kisha kinasibu alichagua vikaratasi kumi na moja ili kupata idadi ya nyimbo za singeli zilizotumika katika makala haya. Data katika nyimbo hizo zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya kusimba maudhui. Kwa kutumia mbinu hii tuliweza kufanya yafuatayo; mosi, kuzizoea data kwa kuzisikiliza nyimbo katika mitandao ya kijamii. Pili, tulitengenezea misimbo mbalimbali kwa kuzingatia lengo la makala haya. Tatu, kuunganisha misimbo inayoendana na lengo la makala haya lililokuwa kuchunguza dhima za tasifida kimuktadha katika nyimbo za singeli. Data zilizokusanywa kutoka katika nyimbo za wasanii teule zilichanganuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo kwa sehemu kubwa na mkabala wa kiidadi kwa sehemu ndogo.

## MATOKEO YA UTAFITI NA MAJADILIANO

Data za utafiti zimedhihirisha kuwa, kwa kiwango kikubwa tasifida zilizotumiwa katika nyimbo teule za singeli zina dhima kubwa katika kudumisha uhusiano na mawasiliano katika jamii. Makala haya yamewasilisha dhima mbalimbali za tasifida kimuktadha katika nyimbo za singeli kama ifuatavyo:

### Kuonesha Hali Halisi ya Kukosekana kwa Upendo na Heshima katika Ndoa

Dhima hii imedokezwa na tasifida 'anadanga' ambayo imetumika kuonyesha mwanamke afanyaye umalaya. Hii imebainishwa katika utafiti huu kupitia wimbo wa "Siponaye" kwa kumuonesha mwanamke ambaye amekosa upendo na heshima ya kutulia katika ndoa yake na badala yake amekwenda kudanga kwa wanaume wengine kiasi cha kushindwa kuendelea kuishi naye. Kukosekana kwa uaminifu katika ndoa hutikisa kiini cha umoja katika ndoa (Chapman, 2008). Hili limebainishwa kupitia nukuu ifuatayo ya wimbo wa "Siponaye" (2021) wa Manfongo:

> *Nasema na watoto wa Libya shemeji yenu sipo naye,*
>
> *Nasema na nyie mahome boy shemeji yenu sipo naye,*
>
> *Na atakaemkuta na bwana niliaacha achana naye,*
>
> *Atakayekutana* ***anadanga*** *nilishabwagana naye,*
>
> *Kwaa sasa nimeghairi namtafuta anipendaye,*
>
> *Sipo naye, sipo naye sipo naye sipo naye,*
>
> *Ninadoonda kubwa chanzo ni ex,*
>
> *Nahisi sitapenda tena likiwa donda ndugu,*
>
> *Kweli sitapenda tena kama nilivvyomuhusudu,*
>
> *Licha ya kumuonesha mapenzi yangu,*
>
> *Hana thamani kwangu,*
>
> *Ila poa tu yote namuachia Mungu,*
>
> *Nilimsihi atulie, kilichopo tutumie kisichokuwepo tutatafuta,*
>
> *Yote namuachia mungu,*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1470

Dondoo hapo juu linamuonesha mwanamke ambaye haheshimu ndoa yake na badala yake anadanga mtaani. Msanii wa wimbo wa “Siponaye” (2021) anaeleza kwamba marafiki zake wasishangae wakimkuta mke wake na mwanamume mwingine kwa vile walishaachana kutokana na kukosa maadili katika ndoa. Msimbo wa kirejelezi wa nadharia ya Semiotiki umetuongoza kubaini kuwa tasifida ya ‘kudanga’ katika muktadha wa ndoa inarejelea hali ya mwanamke kuwa Malaya. Umalaya wa mwanamke huyu umemfanya awe na dharau hali inayomfanya ashindwe kutambua wema wowote uliofanywa na mume kwa kukiuka miiko na tamaduni za jamii yake. Data ya utafiti huu, inafanana na mawazo ya Charles (2008) anayedai kuwa asasi ya ndoa inakumbwa na changamoto nyingi zinazotokana na uasherati, wivu pamoja na matatizo ya kifedha. Hii inaonesha wazi kuwa ili upendo udumu katika ndoa ni lazima suala la uchumi na masuala ya kisaikolojia baina ya mke na mwanamume yawe vizuri kwani ndiyo yanaweza kuwaunganisha.

### Kubainisha Kazi Zisizo Halali katika Jamii

Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa nyakati za usiku si sawa na nyakati za mchana kwa sababu dhima ya kufanya kazi mchana hulenga kuonesha kazi halali wakati nyakati za usiku hutumiwa kufanya kazi zisizo za kihalali. Hii ni kwa sababu mchana kuna nuru, hivyo, maovu mengi hufichwa, hayafanyiki hadharani. Kupitia wimbo wa “dada Asha” tumebaini kwamba tasifida ya **kudanga** inapewa mashiko sana nyakati za usiku kwa maana kwamba watu wanakuwa huru kufanya maovu katika miktadha yenye giza. Aidha, kutokana na tabia za wanawake hawa wanaojiuzai wanapokutana na wanamume, ni rahisi sana kwa wanamume wasio na msimamo kupoteza mwelekeo wa maisha, kazi hata familia zao. Halikadhalika, msimbo wa kiurejelezi umetuongoza kubaini kuwa tasifida ya ‘kudanga’ inarejelea kazi za hatari zinazofanywa nyakati za usiku na katika mazingira yaliyojificha kama anavyoeleza msanii Manfongo katika wimbo wa “dada Asha” (2021) katika ubeti ufuatao.

*Mishe zake dada Asha usiku ni za* ***kudanga,***

*Ukija kichwa kichwa mwanangu atakutia chaka,*

*Anapenda mchezo wa kuringa ringa,*

*Anapenda mchezo wa kujishaua,*

*Mishe zake usiku dada Asha ni za* ***kudanga*** *aaaa,*

*Ukiingia kichwakichwa atakupiga changaaaaa,*

Katika wimbo huu, tumeona kuwa tasifida ya ‘kudanga’ katika muktadha wa giza imetumiwa kwa dhima ya kudokeza kazi inayofanywa usiku na dada Asha. Kazi hiyo ya kudanga huwapotezea mielekeo ya maisha wanaume wote wanaoshindwa kuchukua tahadhari kwa kujihusisha na wanawake wadangaji. Fakih (2017) anashadidia kwamba baadhi ya wanaume wamekuwa wakiwaona wanawake wanaweza kumaliza kiu yao hasa katika masuala ya mapenzi. Hali ya wanaume kuhitaji kumaliza kiu yao ya kimapenzi huwafanya wanaume kujihusisha na masuala ya mapenzi na wanawake bila uchunguzi wala tahadhari na kujikuta wakidanganywa na kudhulumiwa na wanawake wanaojiuza nyakati za usiku.

### Kuweka Wazi Maumbile ya Mwanadamu na Utofauti wake katika Utendaji

Hii ni dhima nyingine ya tasifida ambayo imejitokeza katika wimbo uitwao “Spesho” (2018) wa Manfongo na wimbo wa “Kipusa” (2021) wa Msagasumu. Katika muktadha wa nyimbo teule kumetumika tasifida za dodoki na vibamia ambazo zimedokeza maumbile ya wanaume, yaani dodoki kurejelea dhakari kubwa na vibamia kurejelea dhakari ndogo. Maumbile haya yamedokezwa kuonyesha utofauti wa utendaji kazi wake katika tendo la ndoa. Hili tunaliona katika ubeti ufuatao wa wimbo wa “Kipusa”:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1470

*Hakuna mwingine sifa zako chukua,*

*Mi love ya kweli mpaka siku naumia,*

*Mimi* ***dodoki*** *achana na* ***vibamia,***

*Mimi mtoto wa uswazi kwako natangaza nia,*

*Kangekuwa kanapenda spesho ningekaona kariakoo,*

*Lakini mapenzi mchumba noo, akijitupia anatoka bomba,*

Kupitia dondoo hapo juu, tunaona dhima ya tasifida ya 'dodoki' na 'vibamia' katika muktadha wa mapenzi. Lengo la tasifida hii ni kudokeza utendaji kazi wa kiungo cha mwanamme wakati wa tendo la ndoa. Aidha, imebainika kuwa ishara ya 'dodoki' katika muktadha wa kimapenzi inawasilisha dhakari kubwa yenye uwezo katika tendo la ndoa na ishara ya 'vibamia' inawakilisha dhakari ndogo ya mwanamume isiyo na uwezo wa kuwaridhisha wanawake katika tendo la ndoa.

Pia, katika wimbo wa "Kipusa" ulioimbwa na Msagasumu kuna matumizi ya ishara ya dodoki inayoonesha utofauti wa kiungo na umbile la mwanamume katika utendaji wa tendo la ndoa. Hili limebainishwa na mtafiti kupitia wimbo wa "Kipusa" (2021) wa msanii Msagasumu katika beti zifuatazo hapa chini:

*Sifa wanazitambuaa, mwili wakiusugua,*

*Wengine wanalitaka lakini linawachubua,*

*Dodoki langu mie, wanalipenda wenyewe,*

*Dodoki langu mie wanalipenda wenyewe.*

*Majirani wanataka kulitumia, asirani siwezi,*

*Kuwapatia, majirani wanataka kulitumia,*

*Asirani siwezi kuwapatia dodoki langu mie,*

*Wanalipenda wenyewe, dodoki langu mie,*

*Wanalipenda wenyewe.*

Beti hizo zimeonesha kuwa dhima ya matumizi ya dodoki na vibamia katika muktadha wa kimapenzi ni kudokeza namna tendo la ndoa linavyoweza kufanyika katika hali ya kumridhisha mwanamke. Kutokana na mwanamume kuwa na uwezo mzuri wa kufanya tendo la ndoa, huwavutia wanawake wengi kiasi cha kuanza kumgombania hata kama ni mume wa mtu. Hii inatokana na sababu kwamba katika muktadha wa kimapenzi tasifida ya dodoki inarejelea dhakari kubwa ya mwanamume inayomwezesha kuwa bora wakati wa utendaji wa tendo la ndoa.

**Kuonesha Ugumu wa Maisha**

Katika wimbo wa "Muacheni Adange" tumebaini kuwa miongoni mwa dhima ya tasifida ni kudokeza ugumu wa maisha katika jamii licha ya kupitia mambo yanayoumiza. Tasifida iliyotumika katika kudokeza maumivu ni 'muacheni adange'. Katika utafiti huu tumebaini kuwa wazazi ni chachu kubwa ya kuwafunza watoto wao umuhimu wa kuyabeba mambo magumu na kusonga mbele. Pia, wakati mwingine hufanya kazi za kujidhalilisha kwa ajili ya kuwatunza na kuwalea watoto wao badala ya kuwatelekeza na kuwatupa. Hili limethibitishwa kupitia wimbo wa "Muacheni Adange" (2017) wa msanii Msagasumu kupitia beti za wimbo huo:

*Hana baba wala mama,*

*Ana watoto watano wote wanamtegemea,*

*Kula yao jamani shida,*

*Yuko peke yake hakuna wa kumsaidia.*

*Muacheni* ***adange,*** *muacheni* ***adange,***

*Muacheni* ***adange,*** *muacheni* ***adange.***

*Nashangaa majirani akitoka wanamsema,*

*Akirudi wanamsema hawajui tabu anayopata yule,*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1470

*Na watoto wake, hawajui shida anazopaata*

*Na familia yake,*

*Muacheni* ***adange,*** *muacheni* ***adange,***

*muacheni* ***adange.***

*Kula yao wanamuangalia yeye,*

*Kuvaa yao wanamuangalia yeye,*

*Shule yao wanamuangalia yeye,*

*Kwa nini* ***asidange eee,***

***M****uacheni* ***adange, adange*** *mama,*

*A****adange m****ama,* ***adange*** *mama.*

Katika dondoo hilo hapo juu, tumebaini kuwa tasifida ya **kudanga** katika muktadha wa kifamilia inarejelea shughuli zinazofanywa na wanawake katika kujikwamua kiuchumi kwa ajili ya kulea watoto waliotelekezwa na baba zao. Aidha, njia pekee aliyoichagua mama wa watoto watano ni kuamua kufanya shughuli ya kuuza mwili wake kwa lengo la kujikwamua kiuchumi ili aweze kuwasomesha na kuwalisha watoto. Hali hii inasababishwa na ugumu wa maisha wanayokabiliana nayo wanawake katika kuwalea watoto wao kwa sababu ya kukosa wanaume wa kushirikiana nao katika malezi.

**Kuibua Tabia Zisizokubalika katika Jamii**

Utafiti huu umebaini kuwa tasifida nyingi katika muktadha wa kijamii zinatweza nafasi ya mwanamke katika jamii. Mwanamke anafahamika kama mlezi na mhimili katika familia lakini katika utafiti huu tumeona wanawake wakifanya matendo ya uovu na kushindwa kusimama katika nafasi zao. Kwa mfano, wimbo wa "Chawa" unamuonesha mwanamke kuwa chombo cha starehe kwa kufanya ngono na kila mwanamume hadi kuitwa chakula cha wahuni. Kupitia wimbo wa "Chawa" msanii anahimiza juu ya umuhimu wa kuishi maisha halisi na halali. Anapiga vita mtu kuishi maisha ya kujionesha kwamba ana pesa wakati anaishi kwa madeni pamoja na kufanya kazi zisizo halali kama za kujiuza mwili. Hili limebainishwa na wimbo wa Manfongo uliojulikana kwa jina la "Chawa" (2021) kupitia beti zifuatazo:

*Kumbe chawa huyoooo, amezua kizazaaa*

*Kumbe chawa huyo, na madeni kila baaa,*

*Kumbe chawa huyoooo,*

*Huyo jamani balaa kumbe chawa huyooo,*

*Oneeni wanamshangaa kumbe chawa huyooo,*

*Uchawaa wake unampa thamani,*

*Ndo yule kidemu cha masikani,*

***Ndo yule chakula cha wahuni,***

*Usijie boss we sio boss unayumba,*

*Unapenda unywanywa mwanangu unayumba,*

Katika nukuu hiyo tasifida ya 'chakula cha wahuni' imetumiwa katika wimbo wa "Chawa" (2021). Tasifida hii ya chakula cha wageni katika muktadha wa baa imechorwa kitaswira kwa dhima ya kuwakilisha mtu anayejifanya ana maisha mazuri kumbe anafanya kazi kujiuza mwili wake kwa wanaume tofauti tofauti. Aidha, utafiti huu umebaini kuwa suala la mwanamke kutambua nafasi yake katika jamii ni la msingi katika maisha kwani kwa kiasi kikubwa jamii bora itajengwa na wanawake kwani ndio wanaobeba suala la malezi katika jamii. Si hivyo tu, bali wanawake ndiyo kilele cha uchumi licha ya kuchukuliwa duni kutokana na jinsia yao (Wasike, 2020). Kadhalika, msimbo wa kiurejelezi umetuongoza kubaini kuwa tasifida ya 'chakula cha wahuni' inarejelea wanawake wanaouza miili yao kwa ajili ya kujitafutia kipato na maisha mazuri kwa haraka ambapo ni kinyume na maadili ya jamii.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1470

**Kukemea Mmomonyoko wa Maadili katika Jamii**

Mmomonyoko wa maadili ni hali ya kupotea kwa maadili mionongoni mwa kundi au mtu binafasi katika jamii (Masath, 2013). Kulingana na mabadiliko na maendeleo ya sayansi na teknolojia, jamii inakumbwa na wimbi kubwa la kupotea kwa maadili yanayofaa (Possi, 1996). Kutokana na hali hiyo, imebainika kuwa yapo mambo ya kimaadili yasiyoweza kutamkwa moja kwa moja kutokana na miiko ya jamii. Hivyo, wasanii hutumia tasifida katika muktadha wa matumizi ya vilevi kwa lengo la kuyakemea maovu yote ambayo ni chanzo cha mmomonyoko wa maadili katika jamii pamoja na kuionya jamii kuachana nayo kwani hayafai katika jamii. Katika wimbo wa "Hainogi" (2021) msanii anasema:

*Kuvuta mibange kulewa mipombe,*

*Sio sawa hainogi kushika mipanga,*

*Kuiba kuchinja kujifanya jasusi,*

*Kufuga mkongo **kugawa bila kinga**,*

*Kugawa virusi hainogi unadanga danga,*

*Ukipata mimba unaua kijusi hainogi,*

Kupitia nukuu hiyo, tumebaini kuwa suala la maadili katika jamii linapaswa kusimamiwa kwa nguvu na kukemewa vikali. Aidha, msimbo wa kiurejelezi umetuongoza kubaini kuwa tasifida ya 'kugawa bila kinga' imerejelea mwenendo mbovu wa wanaume na wanawake kufanya ngono zembe na kila mtu. Si hivyo tu bali suala la ulevi wa pombe, kushika mapanga, kuiba, kuchinja na kugawa virusi ni miongoni mwa masuala yanayoonesha kukosekana kwa maadili katika jamii.

Vilevile, katika wimbo wa "Kitasa" ulioimbwa na Msagasumu imebainika kuwa tatizo la mmomonyoko wa maadili ni kubwa hadi ndani ya ndoa. Mathalani, tasifida ya 'kitasa' imetumiwa kwa dhima ya kuwasilisha wanawake malaya ambao hawatulii na mwanamume mmoja; funguo ni wanaume ambao wanashiriki na kila mwanamke katika kufanya uasherati. Hili limeoneshwa kupitia nukuu za ubeti wa wimbo wa "Kitasa" (2021) kama ifuatavyo:

*Nina **kitasa** changu ndicho kinanipa utata,*

*Nina **kitasa** changu mwenyewe ndicho*

*Kinachochonipa kiwewe, wahuni kitasa changu*

*Kitasa ndo kinachonipa utata,*

*Nina kitasa changu mwenyewe,*

*Ndicho kinachonipa kiwewe.*

*Tatizo **kitasa** changu kila **funguo** inafungua,*

*Msagasumu napata machungu pale ninapokifikiria,*

*Hakichagui fungua hicho, kila aina inaingia,*

*Kweli **kitasa** changu sio, ndio maana naibiwa,*

*Akili inaniuma Msagasumu nishamwaga mapesa.*

Nukuu hapo juu imeonesha wazi kuwa tasifida ya kitasa na funguo katika muktadha wa kimapenzi inashiria uke wa mwanamke kama kitasa na uume wa mwanaume kama funguo. Matumizi ya tasifida hiyo yana dhima ya kuonesha hali ya mmomonyoko wa maadili ulivyo katika jamii na namna unavyopaswa kupigwa vita katika jamii. Hali hii imetokana na kitendo cha mwanamke kushindwa kutulia na mwanamume mmoja wa ndoa kama ilivyowasilishwa katika tasifida ya 'kitasa' kwamba hakichagui 'funguo'. Aidha, msimbo wa kiurejelezi umetuongoza kubaini kuwa tasifida ya 'funguo' inarejelea dhakari ya mwanamume inayotumiwa wakati wa kufanya ngono na mwanamke. Hivyo, hali ya kitasa kuingiliwa na kila ufunguo inarejelea mmomonyoko mkubwa wa maadili uliowakumba wanawake kutokana na kushiriki ngono na kila mwanamume.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1470

### Kuhimiza Umuhimu wa Mapenzi ya Dhati katika Jamii

Dhima nyingine ya tasifida ni ile ambayo imejitokeza katika wimbo wa "Mtoto Mdogo Mdogo" (2021). Katika wimbo huu tasifida ya 'nikune kama nazi' imedokeza kufanyika kwa tendo la ndoa kwa kiasi kinachomridhisha mwanamke. Vilevile, katika wimbo huo tumebaini kuwa katika muktadha wa kimapenzi tasifida zina dhima kubwa katika kuhimiza na kuonesha umuhimu wa mapenzi ya dhati kwa mtu umpendaye hata kama jamii inawatazama tofauti. Data hii inalingana na mawazo ya Earp (2021) anayedai kuwa mapenzi ya kweli huthaminiwa. Katika utafiti huu, hili limejidhihirisha kupitia ubeti wa wimbo wa "Mtoto Mdogo Mdogo" (2021) kama msanii Manfongo anavyoeleza hapa chini:

*Hana ghasighasi, wanafiki mko wapi,*

*Wanafiki ni wengi la azizi mtoto mdogo mdogo,*

*Uzee mwisho Chalinze we nahegema,*

***Nikune kama nazi** laaazizi,*

*Ila tui usimalize we nahegema,*

*Wanasema mtoto mdogomdogo,*

*Nimedata naye, kwenye kuni siri ya mhogo,*

*Siachani naye.*

Dondoo hapo juu inaonesha wazi kuwa katika muktadha wa kimapenzi suala la kuridhishana kati ya mume na mke wakati wa tendo la ndoa ni la muhimu. Msimbo wa kiurejelezi umetuongoza kubaini kuwa tasifida ya 'nikune kama nazi' inarejelea kufanyika kwa tendo la ndoa kwa namna itakayomfanya mwanamke aridhike na kufurahia. Data hii, inalingana na utafiti wa Calvo (2005) anayeeleza kuwa matumizi ya tasifida za kimapenzi huwa na dhima ya kuchochea mwamko wa mapenzi kwa namna ambayo inakubalika na jamii kwa kuonesha hisia za kimapenzi kupitia mazungumzo ya mdomo. Hali hii inadhihirika zaidi kwa watu wawili wanaopendana na kuwa na mapenzi ya dhati licha ya tofauti ya umri katika ndoa kwa wawili wapendanao.

### Kuweka Bayana Uhalisia wa Mwanamume

Mwanaume ni mtu wa kuhangaika katika kutafuta maisha, asiyechoka walakuona aibu wakati wa uwajibikaji (Mohammed, 2018). Utafiti huu umebaini kuwa tasifida zimetumiwa katika muktadha wa nyimbo za singeli kwa dhima yaa kuweka bayana uhalisia wa wanaume. Katika tasifida ya "mwanamume mashine" (2021) Msagasumu anadokeza kuwa uhalisia wa mwanamume ni dhakari, tena dhakari yenye uwezo kama mashine ambayo inaweza kumridhisha mwanamke. Kutokana na kuonyesha uhalisia huo, Msagasumu anapingana na mtazamo wa kumwangalia mwanamume kwa kuzingatia uzuri, unene, wembamba na pesa. Kulingana na tasifida hii, kuwa na pesa au sura nzuri hakumfanyi mtu kuwa mwanamume wa kweli. Ubeti ufuatao unaeleza haya:

*Hii hapa nyingine kwa wasioelewa,*

*Uzuri wa mwanaume, uzuri wa mwanaume,*

*Mwanaume sio sura, mwanaume si uzuri,*

*Mwanaume sio unene, mwanaume si wembamba,*

*Uzuri wa mwanaume, mwanaume si wembamba,*

*Uzuri wa mwanaume, mwanaume ee,*

*Najua mwanaume, mwanaume ee,*

***Mwanaume mashine**, yaani mashine,*

***Mwanaume mashine**, yaani mashine,*

***Mwanaume mashine**, yaani mashine,*

*Kama unataka pesa nenda kwa Manji,*

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1470

*Kama unataka pesa nenda kwa Bakheresa,*

*Mimi maskini kama unanipenda nipende,*

*Kama unanijali nijali, wala mimi sina kitu,*

*Ninachoringia mashine, yaani mashine.*

Katika dondoo hilo tunaona kuwa uhalisia wa mwanamume umejengwa katika mtazamo wa uwezo wake kufanya mapenzi. Hii ni kwa sababu mwanamume mwenye uwezo mkubwa wa kumridhisha mwanamke kingono ndiye mwenye sifa ya uanaume. Halikadhalika, msimbo wa kiurejelezi wa nadharia ya Semeotiki umemwongoza mtafiti kubaini kuwa tasifida ya 'mwanaume mashine' imetumiwa na msanii kurejelea uwezo wa mwanamume wa kingono utokanao na dhakari imara. Bradley (1978) anafafanua zaidi kuwa, mwanaume anapokuwa na uwezo mdogo wa kuzalisha mbegu za uzazi humfanya kuwa dhaifu katika kumridhisha mwanamke. Hivyo, uanaume kwa kuzingatia mtazamo unaojitokeza katika wimbo huu, si pesa au sura bali uwezo wa kutekeleza tendo la ndoa.

## HITIMISHO

Makala hii imejadili dhima za tasifida kimuktadha katika nyimbo za singeli. Imebainika kuwa tasifida katika nyimbo za singeli zinatumika kulingana na muktadha wa msanii. Matokeo yanaonesha kuwa tasifida katika nyimbo za singeli zina dhima mbalimbali kama vile: kuonyesha uhalisia wa mwanamume, kudokeza umuhimu wa mapenzi ya dhati katika jamii, kukemea mmomonyoko wa maadili katika jamii, kudokeza tabia zisizokubalika katika jamii, kudokeza kazi zisizo halali katika jamii na kudokeza kukosekana kwa heshima katika ndoa, kudokeza ugumu wa maisha na kudokeza maumbile ya mwanadamu na utofauti wake katika utendaji. Makala hii imeongeza maarifa katika fasihi ya Kiswahili kupitia kipera cha nyimbo kwa kutambulisha nafasi ya nyimbo za singeli katika jamii tofauti na mitazamo inayozichukulia nyimbo hizo kuwa hazina maadili.

## MAREJELEO


Babbie, E. (1999). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Barthes, R. (1994). *The Semiotic Challenge*. Barkeley and Los Angles: University of California Press.

Blonsky, M. (1991). *On Signs.* Baltimore: The Johns Hopkins University Press.

Bradley, W.G. (1978) Self- Serving Biases in The Attribution process: A Reexamination of The Fact of Fiction Question. *Journal of Personality and Social Psychology*, 36, 56-7.

Calvo, J.J. (2005) *The Language of Sex: Saying and Not Saying*. Valencia: De la Universitat de Valencia, I[st] Edition.

Chandler, D. (2002). *Semiotics for Beginners*. Aberystwyth: Aberystwyth University.

Chapman, G. (2008). *Deserate Marriages. Moving Toward Hope and Healing in Your Relationship.* Chicago: Northfield Publishing.

Charles, Z. (2008). *Introduction to Social Work and Social Welfare*. U. S. A.:Thomson Brooks/Cole.

De Saussure, F. (1996). *A Course of General Linguistics*. New York: McGraw-Hill.

Earp, B. D. (2021). *The Ordinary Concept of True Love*. Oxford: Oxford University Press, in Press.

Fakih, S. J. (2017). *Kutathimini Mabadiliko ya Usawiri wa Mwanamke katika* Riwaya ya *Utengano* na *Kamwe Si Mbali Tena*. [Tasinifu ya Uzamili, haijachapishwa. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania].

Jabir, S. (Mtayarishaji) (2015) "Mkasi, S13E05 with Msagasumu" Inapatikana katika https://youtube.be//21QX9ljuc.


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1470

Khatibu, M. S. (1986). Tamathali za Semi za Kiswahili. *Mulika*, Juz. 18: 1-15.

Lanking (Mtayarishaji) (2019) "Anapoishi Manfong". Inapatikana katika youtube https://youtube.be/fOUxszd4T1.

Masath, F. B. (2013). Moral Deterioration: The Reflection on Emerging Sreet Youth Gangs in Musoma, Tanzania. Academic Research International, 49(1), 101-111.

Mohammed, K. I. (2018). *Kuchunguza Usawiri wa Muhusika Mwanamme katika Riwaya ya Kiswahili: Joka la Mdimu na Watoto wa Mama Nt`iliye*. [Tasinifu ya Uzamili, haijachapishwa. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania].

Mwanisenga, R. (2017). Wasiposhtuka Singeli Watajiua Wenyewe. https://mtanzania.co.tz//wasiposhtuka-singeli-watajiua-wenyewe/?fbclid=IwAR2ntPjsvCf44MThdT87RJAoJgs76_hSkfJA_BkGfe1lzrjxscZqHr550ll.

Ndugo, C.M. (2006). *Uwiano wa Picha na Matini katika Mango ya Matangazo wa Kisemiotiki*. [Tasinifu ya Umahili, haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta].

Pierce, C. (1977). *Semiotics and Signific: The Correspondence between Charles. S. Pierce and Lady Victoria Welby*. Indiana: Indiana University Press.

Possi, M. K. (1996). "Effects of Grug Abuse on Cognitive and Social Behaviours: A potential Problem Among Youth in Tanzania". *UTAFITI* (New Series), 3(1): 111-128.

Silavwe, M. I. (2016). *Mtindo katika Riwaya ya Marimba ya Majaliwa na Edwini Semzaba*. [Tasinifu ya Uzamili, haaijachapishwa. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania].

Wasike, W. W. (2020) "Mwanamke wa Kisasa katika Insha za Kifasihi Magazetini: Mtazamo wa Nadharia ya Upalizi". *Mulika*, Na. 38, 87-104.

Yangi, E. (2015). *Matumizi ya Tamathali za Semi katika Nyimbo za Misiba kwa Jamii ya Wahehe.* [Tasinifu ya Uzamili, haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Dodoma].

Zahoro, S. (2018). *Vionjo vya Fasihi ya Kisasa ya Kiswahili katika Nyimbo za Singeli*. [Tasnifu ya Uzamili, haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Dodoma].

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.